Hakika peponi kuna daraja mia moja kaziandaa Mwenyezi Mungu kwaajili ya wenye kupigana katika njia ya Mwenyezi Mungu kati ya daraja mbili ni kama masafa ya baina ya mbingu na ardhi

Kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- yakwamba Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Amesema: "Hakika peponi kuna daraja mia moja kaziandaa Mwenyezi Mungu kwaajili ya wenye kupigana katika njia ya Mwenyezi Mungu kati ya daraja mbili ni kama masafa ya baina ya mbingu na ardhi".

[Sahihi] [Imepokelewa na Al-Bukhaariy]

Anaeleza Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika hadithi hii kuhusu fadhila za wenye kupigana katika njia yake nakuwa Mwenyezi Mungu kawaandalia peponi daraja mia moja, masafa kati ya daraja mbili ni kama yaliyo baina ya mbingu na ardhi.

http://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3624